



COMMUNITY SERVE AND LIFE SURVIVAL ORGANIZATION (CSLSO)
Contact: info@cslso.or.tz, Web: www.cslso.or.tz, Twitter: @SurveSurvival, Insta: servesurvival. P.O.BOX 215 GEITA

TANGAZO LA NA NAFASI ZA KUJITOLEA

Community Serve and life Survival Origination (CSLSO) ni shirika lisilo kuwa la kiserikali (Non Governmental Organization) lenye usajiri **No. 00NGO/0009517** wa Tarehe 15, February, 2018 chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto (The Ministry of Community Development, Gender and Children) linalo jishughulisha na shughuli za mazingira (Environmental Conservation), maendeleo ya afya ya jamii (Community Health Development) na maendeleo ya jamii (Community Development) ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo vijana ili waweze kujitenegea.

Mradi wa Kujengea Uwezo Vijana (Youth Empowerment)

Katika kuwajengea uwezo vijana, shirika linatangaza **NAFASI 20** kwa vijana ambao wako tayari kujifunza kwa vitendo kazi za uhomeleaji (Workshop Activities). Muombaji **HATAKIWI KULIPIA CHOCHOTE** katika mafunzo haya.

Mambo ya Kuzingatia.

1. Mafunzo haya ni mafunzo ya kujitolea kwa vitendo hivyo mwombaji hatakiwi kulipia chochote, mafunzo yatafanyika bure.
2. Mwombaji awe tayari kujifunza kwa kipindi kisichopungua miezi 3 bila kukosa.
3. Mwombaji awe na umri zaidi ya miaka 18 na awe amemaliza darasa la saba.
4. Kwa kuwa karakana yetu ina mali zinazo hamishika mwombaji atalazimika kuja na barua ya utambulisho kutoka serikali ya mtaa wake.
5. Hakuna malipo atakayo pewa, hivyo atajigharamia usafiri, chakula na huduma zingine za muhimu, atakachopata kwetu ni ujuzi (welding skills).
6. Mwombaji atalazimika kufuata kanuni na taratibu za shirika letu kama zilivyo ainishwa kwenye tovuti yetu.

Ujuzi Atakao Upata.

Atakaye bahatika kuchaguliwa ataweza kujifunza yafuatayo:-

1. Kutengeneza samani zifuatazo kwa kutumia chuma
 - I. Vitanda
 - II. Meza
 - III. Milango
 - IV. Madirisha
 - V. Makabati
 - VI. Shelf
 - VII. Gate
 - VIII. Kutengeneza makrasha
 - IX. Ujuzi wa kukunja still plate kutengeneza tank za illusion
 - X. Viti
 - XI. Na samani nyingine za chuma.

Baada ya mafunzo, wanafunzi watashauriwa kuanzisha vituo vyao cha uhomeleaji na shirika litawaunga mkono itakapobidi. Pia watapewa cheti cha mahudhurio.

Sifa za Mwombaji

1. Awe ni Mtanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi
2. Mwenye ulemavu wa aina yoyote, yatima na wale wanaotoka kaya maskini watapewa kipau mbele.
3. Awe anajua kusoma na kuandika na amemaliza darasa la saba.
4. Awe mtiifu kwa walimu wake na asiwe na kiburi juu ya wakufunzi wake.

Mahitaji

| MAHITAJI MUHIMU | |
|----------------------|---|
| MICHANGO | MAELEZO |
| ADA NA MICHANGO | |
| ADA | Mafunzo yanatolewa bure, hakuna ADA ya kulipia |
| Michango Mingine | Hakuna mchango wowote unao hitajika ili uweze kujiunga |
| Malipo ya fomu | Fomu zinatolewa bure hakuna malipo |
| VIFAA VYA KUJIFUNZIA | |
| Square Pipe | Mwombaji atalazimika kuleta vifaa vya kujifunzia. Hata hivyo samani atakayo itengeneza wakati wa kujifunza itakuwa mali yake. Hivyo ataruhusiwa kuuza, kupeleka nyumbani au kugawa. |
| Nondo | |
| Flat Bar | |
| Still Plate | |
| Welding stick | |
| Grinding Disk | |
| Cutting Disk | |
| Electricity | |
| Others | |

ANWANI NA MAHALA TULIPO

- ☞ Tupo Nyankumbu, kumetazamana na Soko la Nyankumbu maarufu kama **Soko la Jioni** mkabala na Kituo cha Mafuta cha LAKE OIL.
- ☞ Pia tunapatikana kwa tovuti ya www.cslso.or.tz au barua pepe info@cslso.or.tz au Sanduku la posta P.O.BOX 215 Geita, au Piga simu +255755834114, au +255767710320.
- ☞ Kwa maulizo yoyote juu ya swala lolote tuandikie info@cslso.or.tz

NAMNA YA KUOMBA

Rudi mwanzoni kwa Tangazo hili angalia sehemu palipo andikwa “**pakua fomu hapa**” bonyeza sehemu hiyo na pakua fomu hiyo. Utapata fomu ambayo itakuwa katika fomart ya **Micro soft Word**. Jaza fomu hiyo kwa **herufi kubwa** kwa kutumia Komputa (*Fomu zilizo jazwa kwa mkono hazitapokelewa*).

Kisha tuma formu hiyo kwenda kwenye anwani ifuatayo.
youthempowerment@cslso.or.tz.

Kwa wale wasiyokuwa na account, fuata hatua hizi kutuma ombi lako.

1. Nenda kwenye google andika www.cslso.or.tz
2. Angalia upande wa juu utaona sehemu imeandikwa **STAFF MAIL** bonyeza utapata sehemu ya kuweka **email** na **password**
3. **Email: Weka helpinghands2020@cslso.or.tz** na Pasward weka **Cslso2020@**
4. Kisha Tumia email hiyo kutuma fomu yako kwenda youthempowerment@cslso.or.tz.
5. Baada ya masaa 24 utapokea ujumbe unao kutaarifu kuwa maombi yako yamepokelewa.
6. Kwa maulizo yoyote wasiliana nasi kwa anwani info@cslso.or.tz

Alliyu Hausi

For Director of Human Resource and Administration
Community Serve and Life Survival Organization.

Email: allyhaus@cslso.or.tz